## Maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba ya uzinduzi wa Wiki ya India Duninia 2020 (India Global Week 2020)

Wageni waheshimiwa kutoka nyanja zote za maisha, Namaste! Salaam kutoka India. Nawapongeza **India Inc Group** kwa kuandaa hafla hii. Hafla hii ni sehemu ya kazi bora kabisa ambazo India Inc zimefanya kwa miaka kadhaa iliyopita. Hafla zenu zimesaidia kuziweka fursa zilizopo nchini India kueleweka ulimwenguni. Mmesaidia kutengeneza muunganiko imara baina ya India na Uingereza. Ninafuraha kwamba hafla ya mwaka huu imeongeza uwigo wake na kuwafikia washirika wengine pia. Nawapongezeni tena! Natumai mwaka ujao, mtapata fursa pia kuwepo Centre Court na kufurahia Wimbledon.

Marafiki, nyakati hizi, ni muafaka kuzungumzia kuhusu kufufua hali na kuirudisha katika nafasi yake ya zamani. Vivohivyo ni muafaka pia kuunganisha ufufuaji huo na India. Kuna imani kwamba harakati za ufufuaji wa hali ya kidunia utaiweka India katika majukumu ya kiuongozi. Hii naiona imehusiana kwa karibu sana na sababu mbili. Moja ni – Vipaji vya India. Duniani kote, mmeona mchango wa nguvu za kipaji cha India. Hii inajumuisha wataalam bobezi, madaktari, manesi, wataalam wa kibenki, wanasheria, wanasayansi, maprofesa, wafanyakazi wetu hodari. Ni nani awezae kusahau taaluma za wataalam bobezi. Wamekuwa wakionyesha njia kwa miongo mingi. India ni kitivo cha vipaji yaani: Yenye shauku kuchangia. Na daima ipo tayari kujifunza. Kuna muunganiko wa pande mbili ambao ni wa faida kubwa.

Marafiki, Sababu ya pili ni uwezo wa India kufanya mabadiliko na kurudi katika ubora wake tena. Wahindi kwa asili ni wanamageuzi! Historia imeonyesha kwamba India imeshinda kila changamoto, iwe ya kisiasa au ya kiuchumi. India imefanya hivyo kwa dhamira ya mabadiliko na kurudisha hali katika ubora wake. Dhamira hiyohiyo inaendelea hivisasa.

Marafiki, kwa upande mmoja India inapambana vita kali dhidi ya janga la kidunia la maradhi. Ikiwa imeweka mkazo mkubwa katika afya za watu, kwa namna hiyohiyo katika afya ya uchumi. Wakati India inazungumzia kuhusu ufufuaji ni kwamba: Ufufuaji kwa tahadhari, Ufufuaji kwa kujali hali (upendo), Ufufuaji ambao ni endelevu – kwa ajili ya vyote, mazingira na uchumi. Sisi nchini India tunaamini tamaduni ambapo Ulimwengu Asilia (Mother Nature) inaabudiwa na kila mmoja. Nchini India inaaminika kwamba Dunia ni Mamayetu na sisi ni watoto wake.

Marafiki, Katika kipindi cha miaka sita iliyopita, India imepata manufaa makubwa katika maeneo kama: Jumla ya ujumuishwaji wa kifedha. Imeweka rekodi katika ujenzi wa nyumba na miundombinu. Kuweka mazingira rafiki kufanya biashara. Mabadiliko makubwa ya kikodi ikiwa ni pamoja na GST. Mabadiliko katika harakati kubwa kabisa za huduma za afya za duniani - Ayushman Bharat. Mafanikio haya yameweka misingi ya duru inayofuata ya mipango ya maendeleo.

Marafiki, Wahindi wana moyo wa kufanikisha kile kinachoaminika kuwa hakiwezekani. Haishangazi kuwa nchini India, tayari tunaona nyota za kijani (ya mafanikio) linapokuja suala la ufufuaji uchumi. Katika wakati huu wa janga la maradhi, tumetoa nafuu/misaada kwa wananchi wetu na kufanya marekebisho ya kina ya kimuundo. Tunajenga uchumi: Wenye kuzalisha zaidi, Rafiki kiuwekezaji na Wenye ushindani.

Misaada yetu imekuwa makini na imelenga kuwanufaisha zaidi masikini. Shukrani kwa teknolojia, kila senti imewafikia walengwa moja kwa moja. Msaada huo ni pamoja na: kutoa gesi ya kupikia bure, pesa katika akaunti za benki, nafaka za chakula bure kwa mamilioni ya watu na vitu vingine vingi. Mara tu tutakapofungua (Lockdown), tumezindua moja ya mpango mkubwa ulimwenguni wa kazi za umma kutoa ajira kwa mamilioni ya wafanyikazi. Hii haitaongeza tu nguvu ya uchumi wa vijijini, bali pia itasaidia kujenga miundombinu imara vijijini.

Marafiki, India inabaki kuwa moja ya uchumi uliowazi zaidi ulimwenguni. Tunaweka zuria jekundu kwa kampuni zote za ulimwengu kuja na kuwekeza nchini India. Ni nchi chache sana ambazo zitatoa fursa ambayo India imefanya hivisasa. Kuna uwezekano mwingi  na fursa nyingi katika sekta mbalimbali zinazochipuka nchini India. Mabadiliko yetu katika kilimo yanatoa fursa ya kuvutia sana katika uwekezaji kwenye uhifadhi na usafiri na vifaa. Tunafungua milango kwa wawekezaji kuja na kuwekeza moja kwa moja katika kazi ngumu ya wakulima wetu.

Marafiki, Tumeleta marekebisho katika sekta ya MSME.  Sekta inayokuwa ya MSME pia itasaidia viwanda vikubwa. Kuna fursa za uwekezaji katika sekta ya ulinzi. Kwa kupunguza kanuni za uwekezaji (FDI),  moja kati ya majeshi wakubwa ulimwenguni linawaalika kuja na kuwatengenezea bidhaa! Hivisasa, kuna fursa zaidi kwa wawekezaji kibinafsi kuwekeza katika sekta ya anga. Hii itamaanisha upatikanaji mkubwa wa matumizi ya kibiashara wa teknolojia ya anga kwa maslahi ya watu. Sekta ya ufundi na uanzishaji ya India ina kasi nzuri. Kuna soko la mamilioni ya watu waliowezeshwa, wenyeuthubutu! Hebu fikiria bidhaa ambazo unaweza kuzalisha kwa ajili yao.

Marafiki, Janga hili la maradhi kwa maranyingine tena limeonyesha kwamba Afya ya India ni rasilimali sio tu kwa India bali kwa ulimwengu mzima. Imetekeleza jukumu kubwa katika kupunguza gharama za madawa hasa kwa nchi zinazoendelea. Chanjo zilizotengenezwa nchini India zinahudumu theluthi mbili ya mahitaji ya chanjo ya watoto waliopo ulimwenguni. Leo pia, kampuni zetu zinafanya kazi kwa juhudi katika harakati za kimataifa za utafutaji na utengenezaji wa chanjo ya COVID-19. Nina hakika kwamba India itakuwa najukumu muhimu katika uvumbuzi na uzalishaji  wa chanjo hiyo mara tu itakapogunduliwa.

Marafiki, Wahindi 1.3 bilion wametoa wito wa India Yenye Kujitegemea (आत्मनिरभर भारत). आत्मनिरभर भारत inajumuisha uzalishaji wa ndani na matumizi pamoja na mnyororo wa usambazaji

kidunia. Inahusu kujikimu wenyewe na kuzalisha wenyewe (Self-sustaining and self-generating. Tutaweka sera ambayo itaongeza ufanisi, uthabiti na uhimili.
Marafiki, nimefurahi kujua kwamba Mkutano huu pia unaadhimisha kumbukumbu ya miaka 100 ya kuzaliwa kwa **Pandit Ravi Shankar**. Alichukua uzuri wa muziki wa asili wa India na kuufikisha ulimwenguni. Pia waweza kuona jinsi Namaste ilivyokwenda ulimwenguni kama namna ya kusalimiana. Janga hili la maradhi pia limefanya Yoga kuwa na thamani, Ayurveda na dawa za kitamaduni katika ulimwengu mzima. Tamaduni za kale za India, Silka za Amani, kilimwengu, ni nguvu yetu.

Marafiki, India iko tayari kufanya kila iwezalo kuendeleza mazuri ya dunia na mafanikio. Hii ndiyo India ambayo inabadili, inafanya na kurekebisha. Hii ndiyo India ambayo inatoa fursa za kiuchumi. Hii ndiyo India ambayo imechagua kuthamini utu na maendeleo jumuishi.

India yawasubini nyote!

Namaste! Asanteni sana.